TANGAZO LA SERIKALI Na. 714 La Tarehe 22/9/2023

SHERIA YA MAJINA YA BIASHARA,
(SURA 213)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 22)*

KANUNI ZA UMILIKI MANUFAA ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA

3. Rejesta ya wamiliki manufaa wa ubia.
4. Taarifa za wamiliki manufaa.
5. Mabadiliko ya wamiliki manufaa.
6. Ukomo wa umiliki manufaa.
7. Zuio la utoaji taarifa za wamiliki manufaa.

SEHEMU YA TATU
REJESTA YA WAMILIKI MANUFAA

8. Rejesta ya wamiliki manufaa.
9. Kukataliwa usajili.
10. Uwasilishaji wa nyaraka.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI MBALIMBALI

11. Makosa na adhabu.
12. Kuongeza muda wa uwasilishaji taarifa.
13. Usiri wa Taarifa.

JEDWALI

SHERIA YA MAJINA YA BIASHARA,
(SURA 213)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 22)*

KANUNI ZA UMILIKI MANUFAA ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Umiliki Manufaa za Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitajika vinginevyo-

"maslahi ya manufaa" maana yake ni maslahi ya kiuchumi au faida au uwezo wa kufanya maamuzi katika ubia;

"mbia mtendaji" maana yake ni mbia ambaye amekasimiwa jukumu la kusimamia shughuli za kiutendaji za ubia;

Sura ya 423

"mmiliki manufaa" itakuwa na maana kama ilivyotolewa kwenye Sheria ya Utakatishaji Fedha;

"mmiliki manufaa halisi" maana yake ni mtu asilia mwenye kumiliki au anayemiliki maslahi ya manufaa katika ubia;

"mmiliki manufaa asiye halisi" maana yake ni mtu asilia mwenye kumiliki au anayemiliki maslahi ya manufaa katika biashara inayoendeshwa kwa ubia pasipo jina lake kuonekana kwenye majina ya wabia;

Sura ya 213

"Msajili" maana yake ni Msajili wa Majina ya Biashara aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Majina ya Biashara;

"ubia" maana yake ni muunganiko wa chombo ambacho hakina utu wa kisheria kinachojumuisha watu wawili au zaidi, au shirika moja na mtu mmoja au zaidi au kampuni moja na mtu mmoja au zaidi au

shirika moja au zaidi ambayo yameingia katika ubia kwa lengo la kufanya biashara kwa faida;

"umiliki usio wa moja kwa moja" maana yake ni umiliki manufaa usio halisi; na

"umiliki wa moja kwa moja" maana yake ni umiliki manufaa halisi.

## SEHEMU YA PILI
## TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA

Rejesta ya taarifa za wamiliki manufaa wa ubia

3.-(1) Kila mbia mtendaji wa jina la biashara linalomilikiwa na wabia atatakiwa kuandaa na kutunza rejesta ya taarifa za wamiliki manufaa wa jina la biashara.

(2) Mbia mtendaji atahakikisha anachukua hatua stahiki kutambua wamiliki manufaa wa ubia na kuingiza taarifa zao katika rejesta ya taarifa za wamiliki manufaa.

(3) Mbia mtendaji atahakikisha kuwa taarifa katika rejesta ya wamiliki manufaa ni sahihi na za wakati kwa muda wote.

Taarifa za mmiliki manufaa

4.-(1) Mbia mtendaji, kwa kuzingatia masharti ya Sheria, atawasilisha kwa Msajili taarifa za mmiliki manufaa. zilizoandaliwa na kutunzwa chini ya kanuni ya 3 kupitia Fomu Na. UM-1 iliyoainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi.

(2) Taarifa zilizorejewa katika kanuni ndogo ya (1) zitawasilishwa kwa Msajili kwa kuzingatia utaratibu ulioelekezwa kwenye mfumo wa upokeaji wa taarifa za umiliki manufaa ndani ya siku sitini kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi kwa ubia uliosajiliwa kabla ya Kanuni hizi na siku thelathini kwa ubia utakaosajiliwa baada ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi.

(3) Mbia mtendaji wa jina la biashara linalomilikiwa na wabia ambao ni wamiliki manufaa halisi, atapaswa kuwasilisha taarifa za wabia hao kwa Msajili kwa kuzingatia utaratibu ulioelekezwa kwenye mfumo wa upokeaji wa taarifa za umiliki manufaa.

(4) Mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki halisi wa manufaa, atawasilisha tamko kuhusu mmiliki halisi wa manufaa kwa mbia mtendaji kwa kujaza Fomu Na.UM-2 iliyoainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi.

*Tangazo la Serikali Na. 714 (Linaendelea.)*

T.S. Na. 127 la mwaka 2014

(5) Mmiliki manufaa halisi ambaye siyo mbia aliyesajiliwa atawasilisha taarifa za umiliki manufaa wake kwa mbia mtendaji kwa kujaza Fomu Na.UM-3 iliyoainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi.

(6) Mbia mtendaji atakayeshindwa kuwasilisha fomu ndani ya muda uliobainishwa chini ya kanuni hii atawajibika kulipa ada ya ucheleweshaji kwa Msajili kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Majina ya Biashara (Ada zinazolipwa kwa Msajili) za mwaka 2014.

Mabadiliko ya wamiliki manufaa

5.-(1) Endapo yatatokea mabadiliko ya umiliki wa maslahi ya manufaa, mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa, atapaswa kuwasilisha taarifa za mabadiliko hayo kwa mbia mtendaji kwa kujaza Fomu Na.UM-2 kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya mabadiliko hayo.

T.S. Na. 127 la mwaka 2014

(2) Mbia mtendaji atatakiwa, baada ya kulipa ada kama zilivyoanishwa kwenye Kanuni za Majina ya Biashara (Ada zinazolipwa kwa Msajili), za mwaka 2014 kuwasilisha kwa Msajili taarifa za mabadiliko ya-

(a) mmiliki manufaa asiye halisi; au

(b) mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi,

kwa kujaza Fomu Na. UM-4 iliyoainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya mabadiliko.

(3) Endapo kutatokea mabadiliko ya muundo wa ubia yenye kuathiri umiliki manufaa, mbia mtendaji atapaswa, kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kwenye Sheria, kuwasilisha kwa Msajili notisi ya mabadiliko kwa kujaza Fomu Na. UM-4 iliyoainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi ikionesha mabadiliko ya muundo wa ubia.

(4) Notisi ya mabadiliko ya umiliki manufaa iliyorejewa katika kanuni hii itasainiwa na mbia mtendaji au mbia aliyekasimiwa majukumu ya mbia mtendaji na kuiwasilisha kwa Msajili.

Ukomo wa umiliki manufaa

6.-(1) Endapo utatokea ukomo wa maslahi manufaa, mbia aliyesajiliwa atapaswa kuwasilisha taarifa za ukomo huo kwa mbia mtendaji kwa kujaza Fomu Na.

UM-2. kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya ukomo huo.

T.S. Na. 127 la mwaka 2014

(2) Mbia mtendaji atapaswa, baada ya kulipa ada kama zilivyobainishwa kwenye Kanuni za Majina ya Biashara (Ada zinazolipwa kwa Msajili), za mwaka 2014 ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kukoma umiliki manufaa, kuwasilisha taarifa kwa Msajili kuhusu ukomo wa-

(a) mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi; au
(b) mmiliki manufaa halisi,

kwa kujaza Fomu Na. UM-5 iliyoainishwa kwenye Jedwali katika Kanuni hizi.

Zuio la utoaji taarifa za wamiliki manufaa.

7. Mbia mtendaji na wabia wenza hawatatumia au kutoa taarifa yoyote kuhusu mmiliki manufaa isipokuwa-

(a) kwa ajili ya mawasiliano na mmiliki manufaa husika;
(b) kwa ajili ya kutekeleza hitaji la Sheria;
(c) kutekeleza amri ya mahakama;
(d) kutekeleza maelekezo ya mmiliki manufaa husika; au
(e) kutekeleza mahitaji ya sheria nyingine.

## SEHEMU YA TATU
## REJESTA YA WAMILIKI MANUFAA

Rejesta ya wamiliki manufaa

8.-(1) Kutakuwa na rejesta ya wamiliki manufaa itakayoanzishwa na kutunzwa na Msajili.

(2) Rejesta itakayoanzishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itahifadhi taarifa za wamiliki manufaa wa jina la biashara zilizowasilishwa kwa Msajili kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(3) Taarifa za wamiliki manufaa wa jina la biashara linalomilikiwa na wabia zilizohifadhiwa na Msajili kwenye rejesta ya wamiliki manufaa zinaweza kutolewa kwa mamlaka idhinishwa zilizoainishwa katika kifungu cha 21 cha Sheria baada ya kuwasilisha kwa Msajili maombi kwa njia ya maandishi.

Kukataliwa usajili

9.-(1) Msajili anaweza kukataa kusajili nyaraka

yoyote ya jina la biashara inayopaswa kusajiliwa chini ya Sheria ikiwa-

(a) taarifa za mmiliki manufaa hazikuwasilishwa; au

(b) hakuridhishwa na usahihi wa taarifa iliyowasilishwa na mbia mtendaji kuhusu wamiliki manufaa wa jina la biashara.

(2) Endapo Msajili atakataa kusajili nyaraka kwa mujibu wa kanuni hii, atapaswa kuwajulisha wahusika kuhusu uamuzi huo.

Uwasilishaji nyaraka

10. Nyaraka inayopaswa kuwasilishwa kwa Msajili chini ya Kanuni hizi, inaweza kuwasilishwa katika muundo na kwa utaratibu utakaojumuisha muundo wa kielektroniki na mawasiliano kwa njia ya kielektroniki kama ambavyo Msajili atakavyoona inafaa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MBALIMBALI

Makosa na adhabu.

11. Mbia mtendaji, mbia mwenza au mtu yeyote ambaye-

(a) atashindwa kutunza kumbukumbu za wamiliki manufaa;

(b) atashindwa kuwasilisha kwa Msajili tamko lenye taarifa za wamiliki manufaa; au

(c) atakiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi,

atakuwa ametenda kosa na endapo akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano.

Kuongeza muda wa uwasilishaji taarifa

12.-(1) Endapo muda wa uwasilishaji taarifa umeainishwa chini ya Kanuni hizi, na endapo itatokea Mbia mtendaji ameshindwa kuwasilisha taarifa husika ndani ya muda ulioainishwa, Mbia mtendaji anaweza, kabla ya muda ulioainishwa wa uwasilishaji haujaisha, kuomba kwa Msajili muda wa nyongeza ili aweze kuwasilisha taarifa hizo.

(2) Msajili anaweza, endapo atajiridhisha na sababu zilizotolewa kwenye ombi lililowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), kuongeza muda ulioombwa kwa kipindi kisichozidi siku thelathini.

Usiri wa taarifa

13. Msajili, afisa yeyote anayetekeleza majukumu chini ya Sheria, hataruhusiwa hata baada ya ukomo wa ajira, kuweka wazi au kutoa taarifa zilizopatikana kwa mujibu wa Kanuni hizi kwa mtu yeyote ambaye hajaidhinishwa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 4(1)), 4(4), 5(1) na 6(1), 4(5), 5(2) na (3), 6(2))*

FOMU

FOMU Na. UM-1

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
SHERIA YA MAJINA YA BIASHARA
TAARIFA ZA MMILIKI MANUFAA

*(Imetengenezwa chini ya kanuni 4(1))*

Taarifa za Jina la Biashara

| | |
|---|---|
| Jina la Biashara | |
| Namba ya usajili | |
| Anwani ya ofisi | |

Mbia Mtendaji wa Jina la Biashara tajwa hapo juu anawasilisha taarifa za mmiliki manufaa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213 na kanuni ya 4(1) kama ifuatavyo:

Tarehe ya kuanza kuwa mmiliki manufaa ………./……………../……………….. (tarehe/mwezi/mwaka)

(a) Mmiliki Manufaa:

| | | |
|---|---|---|
| Jina Kamili (*taja jina lolote la zamani au jingine /mengineyo*) | | |
| Tarehe na mahali pa kuzaliwa | | |
| Mahali pa kazi na cheo chako | | |
| Uraia na Utambulisho | Uraia | |
| | Aina na namba ya utambulisho Mf. | |
| | Tarehe ya kuisha muda wa kitambulisho | |
| | Mamlaka na Nchi iliyotoa kitambulisho | |
| Anwani ya makazi na posta, baruapepe na namba ya simu | Jina la jengo /Namba ya kiwanja | |
| | Mtaa | |
| | Kata | |

| | | |
|---|---|---|
| | Wilaya | |
| | Mkoa | |
| | Nchi | |
| | Msimbo wa Posta | |
| | Baruapepe | |
| | Anwani ya posta | |
| | Namba ya simu | |
| Tarehe ya tamko (Tarehe/Mwezi/Mwaka) | | |
| Tarehe ya tamko kupokelewa na Mbia Mtendaji(Tarehe/Mwezi/Mwaka) | | |

(b) Kiwango cha Maslahi au Udhibiti alionao mmiliki manufaa kwenye Jina la Biashara:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ushiriki katika masuala ya kufanya maamuzi | moja kwa moja | ……………………..% | |
| | zisizo za moja kwa moja | ……………………..% | |
| Kiwango cha uwekezaji kwenye ubia | moja kwa moja | ……………………..% | |
| | zisizo za moja kwa moja | ……………………..% | |
| Kiwango cha faida kwenye ubia | moja kwa moja | ……………………..% | |
| | isiyo ya moja kwa moja | ……………………..% | |
| Mipangilio mingine ya kimaslahi katika ubia | Moja kwa moja | Fafanua kwa kiwango gani: | |
| | Isiyokuwa ya moja kwa moja | Fafanua kwa kiwango gani: | |
| Uwezo wa ushawishi au udhibiti mkubwa katika ubia | moja kwa moja | Ndiyo (weka vema) | Hapana (weka vema) |
| | | | |
| | usio wa moja kwa moja | Ndiyo (weka vema) | Hapana (weka vema) |
| | | | |

(c) Uhusiano w a mmiliki manufaa na mbia aliyesajiliwa:

| | |
|---|---|
| Jina la mbia aliyesajiliwa kwa niaba ya mmiliki manufaa | Uhusiano: |

Orodha ya viambatisho (pale inapohitajika):
Makubaliano ya ubia – lazima*

Tamko:

Taarifa zilizotolewa katika fomu hii, pamoja na viambatisho vyake, ni sahihi na kamili kwa kadiri ya uelewa na ufahamu wangu.

(d) Imewasilishwa na:

*Tangazo la Serikali Na. 714 (Linaendelea.)*

| | |
|---|---|
| Jina: | |
| Wadhifa: (onesha kama ni Mbia Mtendaji/mbia aliyekasimiwa majukumu) | |
| Saini: | |
| Chanzo: (onesha ikiwa taarifa-<br>(a) imetolewa na mmiliki manufaa au mwakilishi aliyeidhinishwa;<br>(b) zimechukuliwa katika Daftari la wamiliki manufaa la wabia; au<br>(c) zimetolewa na mbia aliyesajiliwa) | |

**(Zingatia: Tafadhali weka maelezo ya kila mmiliki manufaa katika fomu tofauti*)

FOMU Na. UM-2

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
SHERIA YA MAJINA YA BIASHARA

TAMKO LA MBIA ALIYESAJILIWA AMBAYE SI MMILIKI MANUFAA
*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 4(4), 5(1) na 6(1))*

1. Taarifa za Jina la Biashara:

| | |
|---|---|
| Jina la Biashara | |
| Namba ya usajili | |
| Anwani ya ofisi | |

2. Taarifa za Mbia aliyesajiliwa ambaye si mmiliki Manufaa:

| | | |
|---|---|---|
| Jina Kamili (*taja jina lolote la zamani au jingine /mengineyo*) | | |
| Tarehe ya kuzaliwa: | | |
| Uraia na Utambulisho | Uraia | |
| | Namba ya utambulisho Uraia/ Hati ya Kusafiria | |
| Namba ya kampuni (kama ni kampuni) au Namba ya usajili (ikiwa ni mashirika mengine) | Jina | |
| | Namba ya kampuni au namba ya usajili | |
| | Tarehe ya usajili | |
| | Mahali kampuni iliposajiliwa | |

3. Tamko:

Kwa mujibu wa kanuni ya *4(4)* mimi ……………………………………………………… ninatamka hapa kwamba aliyetajwa hapa chini anamiliki maslahi ya manufaa katika ubia wa jina la biashara tajwa hapo juu.

| | | |
|---|---|---|
| Jina Kamili (*taja jina lolote la zamani au jingine /mengineyo*) | | |
| Tarehe na mahali pa kuzaliwa | | |
| Mahali pa kazi na cheo chake: | | |
| Uraia na utambulisho | Uraia | |
| | Aina na namba ya utambulisho | |
| | Tarehe ya kuisha muda wa kitambulisho | |

*Tangazo la Serikali Na. 714 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| | Mamlaka na Nchi iliyotoa kitambulisho | |
| Anwani ya makazi na posta, baruapepe na namba ya simu | Jina la jengo /Namba ya kiwanja | |
| | Mtaa | |
| | Kata | |
| | Wilaya | |
| | Mkoa | |
| | Nchi | |
| | Msimbo wa Posta | |
| | Baruapepe | |
| | Anwani ya posta | |
| | Namba ya simu | |
| Tarehe ya tamko (Tarehe/Mwezi/Mwaka) | | |
| Tarehe ya tamko kupokelewa na Mbia Mtendaji(Tarehe/Mwezi/Mwaka) | | |

4. Taarifa za maslahi ya manufaa:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ushiriki katika masuala ya kufanya maamuzi | moja kwa moja | ……………………..% | |
| | zisizo za moja kwa moja | ……………………..% | |
| Kiwango cha uwekezaji kwenye ubia | moja kwa moja | ……………………..% | |
| | zisizo za moja kwa moja | ……………………..% | |
| Kiwango cha faida kwenye ubia | moja kwa moja | ……………………..% | |
| | isiyo ya moja kwa moja | ……………………..% | |
| Mipangilio mingine ya kimaslahi katika ubia | Moja kwa moja | Fafanua kwa kiwango gani: | |
| | Isiyokuwa ya moja kwa moja | Fafanua kwa kiwango gani: | |
| Uwezo wa ushawishi au udhibiti mkubwa katika ubia | moja kwa moja | Ndiyo (weka vema) | Hapana (weka vema) |
| | | | |
| | usio wa moja kwa moja | Ndiyo (weka vema) | Hapana (weka vema) |
| | | | |
| Tarehe ya kuanzishwa kwa maslahi manufaa: | | | |
| Sababu za kutosajili ubia kwa jina la mmiliki manufaa: ............................................................... | | | |

*Tangazo la Serikali Na. 714 (Linaendelea.)*

| |
|---|
| Taarifa kuhusu nyaraka/hati, kama ipo, inayoonesha uanzishwaji wa maslahi manufaa: ................. |

Tarehe: ………………………………… Mahali .................................................................

…………………………………………
Saini ya mbia aliyesajiliwa

5. Taarifa za mabadiliko ya umiliki manufaa:
**(Sehemu hii itajazwa pale ambapo yametokea mabadiliko)*

| | |
|---|---|
| Jina Kamili (*taja jina lolote la zamani au jingine /mengineyo*): | |
| Tarehe ya mabadiliko: | |
| Aina ya mabadiliko ya umiliki manufaa: | |
| Maelezo mafupi ya mabadiliko hayo: | |
| Sababu ya mabadiliko: | |
| Taarifa kuhusu nyaraka/hati, kama ipo, inayoonesha mabadiliko ya umiliki manufaa: | |

Tarehe: ………………………………… Tarehe ..................................................

………………………………………… ...............................................................
Saini ya mbia aliyesajiliwa Saini ya mmiliki manufaa

6. Taarifa za Ukomo wa umiliki manufaa:
**(Sehemu hii itajazwa pale ambapo pametokea ukomo)*

| | |
|---|---|
| Jina Kamili (*taja jina lolote la zamani au jingine /mengineyo*): | |
| Tarehe ya ukomo: | |
| Sababu za ukomo: | |
| Taarifa kuhusu nyaraka/hati, kama ipo, inayoonesha ukomo wa umiliki manufaa: | |

Tarehe: ………………………………… Tarehe ..................................................

………………………………………… ...............................................................
Saini ya mbia aliyesajiliwa Saini ya mmiliki manufaa

Viambatisho (pale ambapo inapohitajika):

(a) uthibitisho wa utambulisho wa mbia aliyesajiliwa na mmliki manufaa; na
(b) nyaraka/ hati ambayo kwayo maslahi manufaa yametengezwa/yamehamishwa/ yamebadilishwa/yamekoma.

*Tangazo la Serikali Na. 714 (Linaendelea.)*

FOMU Na. UM-3

JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA
WAKALA WA USAJILI WA
BIASHARA NA LESENI
SHERIA YA MAJINA YA
BIASHARA

TAMKO LA MMILIKI MANUFAA MWENYE MASLAHI KATIKA UBIA
AMBAYE SIYO MBIA ALIYESAJILIWA
*(Limetengenezwa chini ya kanuni 4(5))*

1. Taarifa za Jina la Biashara

| | |
|---|---|
| Jina la Biashara | |
| Namba ya usajili | |
| Anwani ya ofisi | |

2. Taarifa za Mmiliki Manufaa

| | | |
|---|---|---|
| Jina Kamili (*taja jina lolote la zamani au jingine /mengineyo*) | | |
| Tarehe na mahali pa kuzaliwa | | |
| Mahali pa kazi na cheo chako | | |
| Uraia na Utambulisho | Uraia | |
| | Aina na namba ya utambulisho | |
| | Tarehe ya kuisha muda wa kitambulisho | |
| | Mamlaka na Nchi iliyotoa kitambulisho | |
| Anwani ya makazi na posta, baruapepe na namba ya simu | Jina la jengo /Namba ya kiwanja | |
| | Mtaa | |
| | Kata | |
| | Wilaya | |
| | Mkoa | |
| | Nchi | |
| | Msimbo wa Posta | |
| | Baruapepe | |
| | Anwani ya posta | |
| | Namba ya simu | |
| Tarehe ya tamko (Tarehe/Mwezi/Mwaka) | | |

3. Tamko

Kwa mujibu wa kanuni ya 4(5). Mimi ………………… ………..ninatamka kuwa ninamiliki maslahi ya manufaa katika ubia wa jina la biashara tajwa hapo juu kwa jina la mbia aliyesajiliwa ambaye taarifa zake nazitoa hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| Jina Kamili (*taja jina lolote la zamani au jingine /mengineyo*) | | |
| Tarehe ya kuzaliwa: | | |
| Uraia na Utambulisho | Uraia | |
| | Namba ya utambulisho Uraia/ Hati ya Kusafiria | |
| Namba ya Kampuni (kama ni kampuni) au Namba ya Usajili (ikiwa ni mashirika mengine) | Jina | |
| | Namba ya kampuni au namba ya usajili | |
| | Tarehe ya usajili | |
| | Mahali kampuni iliposajiliwa | |

4. Taarifa za umiliki manufaa:

| | | |
|---|---|---|
| Ushiriki katika masuala ya kufanya maamuzi | moja kwa moja | ……………………..% |
| | zisizo za moja kwa moja | ……………………..% |
| Kiwango cha uwekezaji kwenye ubia | moja kwa moja | ……………………..% |
| | zisizo za moja kwa moja | ……………………..% |
| Kiwango cha faida kwenye ubia | moja kwa moja | ……………………..% |
| | isiyo ya moja kwa moja | ……………………..% |
| Mipangilio mingine ya kimaslahi katika ubia | Moja kwa moja | Fafanua kwa kiwango gani: |
| | Isiyokuwa ya moja kwa moja | Fafanua kwa kiwango gani: |

*Tangazo la Serikali Na. 714 (Linaendelea.)*

<table>
<tr><td rowspan="4">Uwezo wa ushawishi au udhibiti mkubwa katika ubia</td><td rowspan="2">moja kwa moja</td><td>Ndiyo (weka vema)</td><td>Hapana (weka vema)</td></tr>
<tr><td></td><td></td></tr>
<tr><td>usio wa moja kwa moja</td><td>Ndiyo (weka vema)</td><td>Hapana (weka vema)</td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="4">Tarehe ya kuanzishwa kwa maslahi manufaa:</td></tr>
<tr><td colspan="4">Sababu za kutosajili ubia kwa jina la mmiliki manufaa: ...............................................................</td></tr>
<tr><td colspan="4">Taarifa kuhusu nyaraka/hati, kama ipo, inayoonesha uanzishwaji wa maslahi manufaa: .................</td></tr>
</table>

Tarehe: ………………………………… Mahali .................................................................

……………………………………………………………………
Saini ya Mmiliki Manufaa

Viambatisho (pale ambapo inapohitajika)*:*

1. Uthibitisho wa vitambulisho vya mmiliki aliyesajiliwa na mwenye haki ya maslahi;
2. Hati/ waraka ambao haki ya maslahi imeundwa/imehamishwa/ imebadilishwa.

FOMU Na. UM-4

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
SHERIA YA MAJINA YA BIASHARA
MABADILIKO YA TAARIFA ZA MMILIKI MANUFAA
*(Imetengenezwa chini ya kanuni 5(2) na (3))*

1. Taarifa za Jina la Biashara

| | |
|---|---|
| Jina la Biashara | |
| Namba ya usajili | |
| Anwani ya ofisi | |

2. Kwa Msajili wa Majina ya Biashara:

Mimi, ........................................................... (Mbia Mtendaji/mbia aliyekasimiwa) wa jina la biashara tajwa hapo juu ninatoa notisi kwa mujibu wa kanuni ya 5(2) na (3) kwamba taarifa zilizosajiliwa kuhusu mmiliki manufaa wa ubia kama alivyobainishwa katika Safuwima ya Kwanza zimebadilika kama ilivyoonyeshwa katika Safuwima ya Pili ya jedwali hili hapa chini:

| Safuwima ya Kwanza<br>Jina la mmiliki manufaa | Safuwima ya Pili<br>Taarifa na tarehe ya mabadiliko |
|---|---|
| | |
| | |
| | |

Orodha ya viambatisho (pale ambapo inapohitajika):

3. Tamko:

Taarifa zilizotolewa katika fomu hii, pamoja na viambatisho vyake, ni sahihi na kamili kwa kadiri ya uelewa na ufahamu wangu.

Imewasilishwa na:

| | |
|---|---|
| Jina: | |
| Wadhifa: (onesha kama ni Mbia Mtendaji/mbia aliyekasimiwa majukumu) | |
| Saini: | |
| Tarehe: | |
| Chanzo: (onesha ikiwa taarifa-<br>(a) imetolewa na mmiliki manufaa au mwakilishi aliyeidhinishwa;<br>(b) zimechukuliwa katika Daftari la wamiliki manufaa la wabia; au<br>(c) zimetolewa na mbia aliyesajiliwa) | |

FOMU Na. UM-5

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
SHERIA YA MAJINA YA BIASHARA
NOTISI YA KUKOMA KUWA MMILIKI MANUFAA HALISI/ MBIA ALIYESAJILIWA AMBAYE SIYO MMILIKI MANUFAA HALISI

*(Imetengenezwa chini ya kanuni 6(2))*

1. Taarifa za Jina la Biashara

| | |
|---|---|
| Jina la Biashara | |
| Namba ya usajili | |
| Anwani ya ofisi | |

2. Kwa Msajili wa Majina ya Biashara

Mimi, ........................................................... (Mbia Mtendaji/mbia aliyekasimiwa) wa Jina la Biashara tajwa hapo juu ninawasilisha taarifa za miliki manufaa/mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi kwa mujibu wa kanuni ya 6(2) kwamba mmiliki manufaa/ mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi katika jina la biashara kama alivyobainishwa katika safuwima ya kwanza ya Jedwali lililoainishwa hapa chini amekoma kuwa mmiliki manufaa/mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi kuanzia tarehe zilizobainishwa mkabala na jina lake katika safuwima ya pili ya Jedwali lililoainishwa hapa chini:

| Safuwima ya Kwanza | Safuwima ya Pili | Safuwima ya Tatu |
|---|---|---|
| Jina la mmiliki manufaa/ mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi | Tarehe aliyokoma kuwa mmiliki manufaa/ mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi | Sababu za kukoma kuwa mmiliki manufaa/ mbia aliyesajiliwa ambaye siyo mmiliki manufaa halisi |
| | ----/----------/-------<br>(Tarehe/Mwezi/Mwaka) | |

Orodha ya viambatisho (kama vipo):

3. Tamko:

Taarifa zilizotolewa katika fomu hii, pamoja na viambatisho vyake, ni sahihi na kamili kwa kadiri ya uelewa na ufahamu wangu.

Imewasilishwa na:

| | |
|---|---|
| Jina: | |
| Wadhifa: (onesha kama ni Mbia Mtendaji/mbia aliyekasimiwa majukumu) | |
| Saini: | |
| Tarehe: | |

*Tangazo la Serikali Na. 714 (Linaendelea.)*

| | |
|---|---|
| Chanzo: (onesha ikiwa taarifa-<br>(a) imetolewa na mmiliki manufaa au mwakilishi aliyeidhinishwa;<br>(b) zimechukuliwa katika Daftari la wamiliki manufaa la wabia; au<br>(c) zimetolewa na mbia aliyesajiliwa) | |

Dodoma,
……………, 2023

ASHATU K. KIJAJI,
*Waziri wa Viwanda na Biashara*